Gloria Mutta, Diwani wa Kata ya Charambe, Twahil Shaban na Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Betha Minga.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

NIPASHE UK 7.

# Wawili mbaroni tuhuma kuvua samaki kwa baruti kilo 980

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kikosi cha Wanamaji jijini Dar es Salaam linawashikilia watuhumiwa wawili wanaodaiwa kukutwa na samaki kilo 980 wanaosadikika kuvuliwa kwa baruti. Kamanda wa kikosi hicho, Moshi Sokoro, alisema jana kuwa samaki hao wamekamatwa wakiwa kwenye boti ya uvuvi yenye namba za usajili Z 103585 MV Maedra.

Alisema wamekamatwa Januari 12, maeneo ya Soko la Samaki Feri baada ya operesheni kufanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Uvuvi na Mifugo.

Kamanda Sokoro aliwashukuru wananchi wanaochukia uhalifu na kuwaomba waendelee kutoa taarifa ili hatua stahiki zichukuliwe.

Alisema Jeshi la Polisi litachukua hatua kwa yeyote atakayehusika na uvuvi haramu pamoja na makosa mengine ya jinai.

CamScanner

HABARI LEO UK 7.

# * Kilo 980 samaki wa baruti wanaswa Feri *

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kikosi cha Wanamaji Dar es Salaam kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi limekamata watuhumiwa wawili wakiwa na samaki kilo 980 waliokuwa ndani ya boti yenye usajili namba Z. 103585, Mv MAEDRA wakisadikiwa kuvuliwa kwa kutumia baruti.

Taarifa iliyotolewa jana na jeshi hilo na kusainiwa na Kamanda wa Kikosi cha Polisi Wanamaji ACP Moshi Sokoro, ilisema boti hiyo ilikamatwa asubuhi ya Januari 12, mwaka huu katika soko la samaki Feri baada ya kufanyika kwa operesheni ya pamoja ya kuzuia uvuvi haramu na makosa mengine ya kijinai.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, taratibu za kuwafikisha watuhumiwa mahakamani zinaendelea huku jeshi hilo likiwashukuru na kuwapongeza wananchi wote ambao wanachukia uhalifu na kuwaomba waendelee kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu ili hatua stahiki zichukuliwe kwa wahalifu hao.

"Pia Jeshi la Polisi linaendelea kutoa onyo kwamba halitasita kuchukua hatua kwa yeyote atakayejihusisha na uvuvi haramu pamoja na makosa mengine ya kijinai," alisema Sokoro katika taarifa hiyo.

CS CamScanner

# Wavuvi Tanga wahofia samaki kutopatikana

Burhani Yakub, Mwananchi
byakub@mwananchi. co.tz

Tanga. Wavuvi wa samaki wamesema upatikanaji wa samaki unaweza kuwa adimu hadi ifikapo Machi mwaka huu kama upepo wa Kaskazi utaendelea kuwa mkali.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, wavuvi hao kutoka Pemkoani Tanga na Kisiwa cha Pemba, walisema upepo unaoendelea baharini hivi sasa ni mkubwa kuliko ilivyokuwa miaka mingine.

Mmoja wa wavuvi hao kutoka Pemba, Nuhu Abdallah alisema upepo wa Kaskazi unaoendelea hivi sasa unaathiri upatikanaji wa samaki.

Alisema kutokana na hali ya bahari kuchafuka, wavuvi wamelazimika kuacha kuingia baharini wakitegea upepo upungue huku akisisitiza kuwa upepo utakwisha Machi.

"Kwa siku za utulivu wa bahari

**"Siku za kawaida huwezi kukaa nusu saa asubuhi bila kusikia muuza samaki akipita nje, lakini hivi sasa zinapita hata siku nne bila kumsikia."**
Kuruthum Ali

wavuvi hufikisha samaki wa uzito wa tani 20, lakini hivi sasa hazifiki hata tani 5, jambo linaloathiri walaji," alisema Nuhu.

Ofisa Uvuvi wa Wilaya ya Tanga, Bagaya Mbwana alisema kuna jumla ya vyombo 800 vya uvuvi, vikiwamo vikubwa na vidogo aina ngalawa na mitumbwi.

Aliwashauri wavuvi, hasa wenye vyombo vidogo vya uvuvi kuacha kwenda bahari ya mbali kwa sababu kuna upepo mkali zaidi.

"Tayari tumeshabandika matangazo kwenye pwani zote zenye vituo vya vyombo vya uvuvi tukiwaeleza kuwa, kwa mujibu wa taarifa za utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) hali ya bahari ina upepo mkali, hivyo wasiende baharini na kama wataenda wasiingie ndani sana na wavae majaketi ya kujiokoa," alisema Mbwana.

Wauzaji wa samaki Kituo cha Deap Sea walisema hivi sasa samaki wameadimika na wanaopatikana ni jodari, sehewa, kolekole, changu na dagaa aina ya uono, tena wasiotosheleza mahitaji ya walaji wa Tanga.



Kwa Ufupi

• NASAHA

NASAHA ZA WIKI

NA THOMAS LAISER
raiatz@gmail.com, 0763102883

# Ajenda 10/30 isiache nyuma wafugaji, wavuvi

KWA wale tunaoamini kuwa utashi wa kisiasa kama kigezo muhimu katika kuharakisha mageuzi ya sekta ya kilimo, tuna haki ya kuamini na kukiri kuwa tupo kwenye kipindi ambacho Serikali imedhamiria kuhakikisha kilimo kinaimarika na kuwa chachu ya ustawi wa maisha ya Watanzania na uchumi wa Taifa kwa jumla.

Kwa uzinduzi wa Ajenda 10/30 uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan Aprili 2022, na kufuatiwa na ongezeko la takriban mara tatu kwa bajeti ya kilimo kama ilivyowasilishwa kwenye Bunge la Bajeti la 2022/23, kisha mfululizo wa matukio mengine ya uhamasishaji yanayoendelea; ni ishara tosha kuwa pana dhamira ya dhati ya kuleta mageuzi ya kilimo nchini.

Kwa wanaofuatilia mwendelezo wa azma hiyo ya serikali, watabaini kwamba; iwapo mipango yote iliyokusudiwa itatekelezwa ipasavyo, basi sio muda mrefu Tanzania itakuwa sehemu ya kupigiwa mfano kwa kuwa nchi ya Afrika iliyoweza kubuni mpango wake wa mageuzi ya kilimo biashara ambao utachochea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi kitaifa.

Mipango kama ile ya kuandaa mashamba ya kuwapatia vijana kupitia mpango wa 'ujenzi wa kesho iliyo bora – (BBT)'; kuwezesha upatikanaji wa mitaji, mbegu, pembejeo, na uvutiaji wa wawekezaji watakaosindika mazao yatakayozalishwa; ni miongoni mwa yale ambayo yakitekelezwa ipasavyo Tanzania itageuka kuwa shamba-darasa kwa mataifa mengine ya bara hili kwa kuonesha njia sahihi kuelekea mapinduzi ya kilimo yanayoongozwa na Waafrika wenyewe!

Lakini, inafahamika kuwa sekta ya kilimo ni sekta pana ikijumuisha shughuli mbalimbali za uzalishaji vijijini. Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO), kilimo kinaelezewa kama jumla ya shughuli zote ikijumuisha uzalishaji mazao, ufugaji na uvuvi. Kwa maana hiyo, jitihada zozote za kuhamasisha ukuaji wa sekta ya kilimo zinapaswa kuzingatia mapana ya sekta husika ili wasiwepo watakaoachwa nyuma.

Wakati wakulima wa mazao wakitabasamu kwa ujio wa Ajenda 10/30, wenzao, yaani wafugaji na wavuvi ni kama wanahisi wamesahauliwa. Ndio maana makala haya yanaonelea ni vema kuwakumbusha watunga sera watambue 'udugu wa damu' uliopo katika sekta hizo na kuwatendea sawa wote wanaojishughulisha nayo, yaani wakulima, wafugaji na wavuvi.

Mchango wa sekta ya mifugo na ile ya uvuvi kwa ustawi wa taifa kiuchumi na kijamii sio haba. Kwenye mkutano Bunge la Bajeti uliomalizika mwishoni mwa Julai 2022, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, aliliarifu Bunge kuwa kwa mwaka 2021-2022, sekta ya mifugo pekee ilichangia asilimia 7.0 kwenye pato la taifa. Mchango huo ulitokana na mauzo ya mifugo na mazao yake.

Wakati ufugaji, ambao kwa zaidi ya asilimia 95 unafanywa na wafugaji wa asili ukitoa ajira kwa maelfu ya Watanzania sambamba na mchango usio haba kwa pato la taifa, mazingira ya ufugaji, hususana ufugaji wa asili yameendelea kuwa magumu kila uchao.

Ni matarajio ya wafugaji kuona ujio wa Ajenda 10/30 ukiwa pia ni fursa kwao ili kuitendea haki sekta hii inayotupa heshima ya kuwa nchi ya pili barani Afrika kwa wingi wa mifugo tukitanguliwa na Ethiopia. Iwapo ufugaji utapewa umuhimu unaostahili, uchangiaji wake kwa pato la taifa unaweza kwenda juu na kushindana na mataifa kama Botswana na Afrika Kusini na hivyo sekta hii kutoa mchango stahiki kwa pato la taifa tofauti na ilivyo sasa.

Ujio wa Ajenda 10/30 usaidie kubadili mtazamo wa baadhi ya watendaji ili, badala ya kujikita kudhibiti mifugo kuvushwa na kuuzwa kwenye minada ya nchi jirani kama vile Kenya, mamlaka husika zijielekeze kuandaa mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara na yatakayonufaisha wafugaji na serikali. Hiyo ni pamoja na kuweka vivutio kwa wale wote wanaotaka kujenga viwanda vya kusindika bidhaa za mifugo kwa lengo la kupanua wigo wa soko la mifugo nchini na kuongeza fursa ya sekta hiyo kukuza uchumi.

Pamoja na hayo, serikali kupitia mamlaka zake, inapaswa kuongeza kasi katika kubaini ardhi za wafugaji na kuhakikisha zinalindwa kisheria dhidi ya uvamizi ambao umekuwa ukifanywa na watumiaji wengine wa ardhi. Hiyo ni pamoja na serikali yenyewe kutoendelea kuongeza ardhi za hifadhi kwa gharama ya kutwaa maeneo ya malisho kwa mifugo.

Kwa upande wa uvuvi, kwa mujibu wa Sensa ya Taifa ya Kilimo 2019/2020, ambayo ilichukua takwimu za kaya zile tu zinazojishughulisha rasmi na ufugaji samaki; ilionesha kuwa kutokana na samaki wafugwao, uzalishaji wa samaki ulikuwa jumla ya tani 12,936. Kati ya hizo, Tanzania Bara uzalishaji ulikuwa tani 12,873 na tani 64 kutoka Tanzania Zanzibar.

Taarifa hiyo ambayo hutoka kila baada ya miaka kumi inabainisha kuwa idadi ya wafugaji wadogo samaki imeongezeka kutoka 10,794 mwaka 2007/08 hadi 26,662 mwaka 2019/20 ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 100.

Kama ilivyo kwa upande wa kilimo cha mazao na ufugaji, kwenye uvuvi nako, ni wavuvi wadogo walioibeba sekta ndogo ya uvuvi hata kama zingelitolewa pia takwimu za mazao ya uvuvi kutokana na vyanzo vya asili ambako kwa uhalisia ndiko wanakopatikana samaki wengi zaidi.

Ni kwamba, hata juhudi kubwa za Serikali zetu zote mbili, Tanzania Bara na Zanzibar, kutaka kuhakikisha kuwa Taifa linawekeza vya kutosha na kunufaika na Uchumi wa Bluu; zinapaswa kuwaweka wavuvi wadogo katikati ya ajenda ya maendeleo ya sekta hiyo wakiwa ndio watekelezaji wakuu.

Inapasa kufahamika kuwa hakuna kinachoitwa mafanikio ya Tanzania kutokana na kilimo, pasipo kutaja mchango wa pamoja wa wafugaji, wavuvi na wakulima wa mazao. Kwa hiyo kama Taifa linachagua kuleta na kufanya mageuzi ya kilimo kupitia Ajenda 10/30, hapana budi kuhakikisha tunawajumuisha pamoja waliomo kwenye sekta hiyo, yaani wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo.

*Mwandishi wa nasaha hizi ni Ofisa Ushawishi na Utetezi-Shirikisho la Vyama vya Wakulima Wadogo Tanzania (SHIWAKUTA)*